## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

### WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

**Telegramu:''LEGAL''**
**Simu Na.:** +255 26 2310019
**Nukushi:** +255 26 2310056
**Barua Pepe:** km@sheria.go.tz
**Tovuti:** www.sheria.go.tz

Mji wa Serikali, Mtumba,
Mtaa wa Katiba,
S. L. P. 315,
**40484 DODOMA.**

10 Desemba, 2025

# TAARIFA KWA UMMA

### SIKU YA KIMATAIFA YA HAKI ZA BINADAMU – 10 DISEMBA, 2025

### Kaulimbiu: "HAKI NA WAJIBU KUELEKEA DIRA 2050"

Leo tarehe 10 Disemba, 2025 Tanzania inaungana na Dunia, kusherehekea Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu, tukikumbuka kwamba haki na wajibu ni msingi wa maendeleo endelevu, mshikamano wa kijamii, na utawala bora. Siku ya tarehe 10 Disemba, ilipitishwa na Azimio la Baraza la Umoja wa Mataifa kuwa Siku ya Haki za Binadamu kwa kuwa ni tarehe ambayo Tangazo la Kimataifa la Haki za Binadamu la mwaka 1948 (Universal Declaration of Human Rights) lilipitishwa na Baraza la Umoja wa Mataifa.

Tangazo la Kimataifa la Haki za Binadamu,1948 ni kati ya nyaraka za awali zinazotambua haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii kama haki za binadamu. Tangazo hilo limeainisha misingi ya haki za binadamu ambayo ni usawa na kutobaguliwa. Kwa muktadha huo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa iliridhia haki zilizo katika Tangazo hilo, ambapo Ibara ya 9(f) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inaelekeza kwamba, heshima ya binadamu inahifadhiwa na kudumishwa kwa kufuata Kanuni za Tangazo la Dunia kuhusu Haki za Binadamu. Hivyo, Serikali ina wajibu wa kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu.

Serikali inatekeleza wajibu huu kwa kushirikiana na wadau wasio wa Serikali wakiwemo wananchi, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Wadau wa Maendeleo pamoja na Mashirika ya Kimataifa na Kikanda. Ushirikiano huu ni utekelezaji wa Ibara ya 29

(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,1977 inayoelekeza kila mtu ana wajibu wa kutenda na kuendesha shughuli zake kwa namna ambayo haitaingilia haki na uhuru wa watu wengine.

Hivyo, Siku hii muhimu inatukumbusha kuwa kulinda na kuenzi haki za binadamu si jukumu la Serikali peke yake, bali ni wajibu wetu sote katika jamii ili kuweza kuboresha uchumi binafsi na kushiriki katika maendeleo ya Taifa. Kwa kuzingatia hili, Serikali iliandaa Dira ya Maendeleo 2050 ambayo misingi yake imejikita katika kuheshimu haki za binadamu ili kulisaidia taifa kuwa na jamii yenye:-

- Usawa, uhuru, na mshikamano;
- Uongozi bora na uwajibikaji; na
- Maendeleo endelevu yanayojumuisha kila mwananchi.

Hii inamaanisha, haki za binadamu na wajibu wa kila raia ni nguzo muhimu za kufanikisha mustakabali ambapo:-

1. Haki za binadamu zinapaswa kuheshimiwa kila wakati. Haki hizi zinajumuisha haki ya kuishi, elimu, afya, usawa, na uhuru wa kiraia.

2. Wajibu wa kila mmoja ni kudumisha utawala wa sheria, kuendeleza mila na desturi nzuri, kuheshimu haki za wengine na kushirikiana katika maendeleo ya kitaifa.

3. Serikali na Taasisi za Umma zinatakiwa kuhakikisha uwazi, uwajibikaji,na utetezi wa haki za binadamu ili kila raia aweze kushiriki kikamilifu katika mustakabali wa Taifa.

4. Wananchi wanatakiwa kuwa mabalozi wa haki na wajibu, kuhakikisha kuwa hakuna mtu anayeonewa, kudhalilishwa, au kushindwa kushiriki katika maendeleo ya Taifa.

Hivyo, leo tunapoikumbuka siku hii, tuwe na moyo wa kulinda haki za kila mmoja na kila mmoja wetu kutimiza wajibu wake tukifanikisha Tanzania yenye mshikamano, amani, usawa, na maendeleo endelevu kuelekea Dira 2050.

**IMETOLEWA NA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**